

Kuvutia, Rezman Ganshonga, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maji inayotekelezwa katika vijiji mbalimbali wilayani Mbinga. (Picha na Muhidin Amri).

kuhakikisha usalama wa chakula unafikiwa nchini.

HABARI LEO UKS

Mifugo 36,000 kuwekewa hereni za kielektroniki

Na Amina Omari, Tanga

MKUU wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa amezindua uwekaji hereni za kielektroniki kwa wanyama kwa lengo la kufanya utambuzi wa wanyama pamoja na kuwa na kanzidata ya mifugo iliyopo.

Akizungumza mara baada ya kufanyika kwa shughuli hiyo katika eneo la Pingoni, Kata ya Maweni

jijini Tanga, Mgandilwa alisema kuwa hatua hiyo itasaidia serikali kujua idadi ya wanyama waliopo nchini na hivyo kurahisisha ugawaji wa dawa na pembejeo za mifugo.

"Kutokana na sisi kuwa katika maeneo ya mipakani, kuna mwingiliano wa wanyama hivyo uwekaji hereni kwa mifuko, kutasaidia kutambua mifugo yetu na itakuwa salama tofauti na sasa," alisema Mgandilwa.

Kwa upande wake Ofisa

Mifugo na Uvuvi wa Hal-mashauri ya Jiji la Tanga, Dk Paul Kisaka alisema katika shughuli hiyo wamejipanga kuwekea hereni mifugo zaidi ya 36,000.

Alisema kuwa kutokana na kuimarisha soko la mazao ya mifugo, uwekaji vifaa hivyo utasaidia kupata uhakika wa masoko ya mazao hayo nje ya nchi.

"Sasa tunakwenda kutambua mifugo ya ndani na nje ya nchi kupitia uwekezaji huu wa hereni za kielektron-

iki lakini itasaidia kuepuka changamoto ya migogoro ya wafugaji na wakulima," alisema Dk Kissaka.

Wafugaji waliozungumzia mkakati huo wa kuwekea mifugo hereni, walisema ni ukombozi dhidi ya wizi wa mifugo ambao umekuwa ni changamoto kubwa kwao.

Mfugaji wa ngombe wa maziwa, Marium Shekue alisema hatua hiyo itasaidia kutatua kero kubwa ya mifugo lakini pia kuimarisha soko la mazao ya mifugo.



SQ011214

* HABARI LEO UK 17 *

Ufugaji samaki wazalisha ajira 729

Na Lucy Ngowi

MRADI wa ufugaji samaki wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, umezalisha ajira 729 baada ya wananchi kupewa mafunzo ya kuendeleza ujuzi yanayotolewa kupitia ruzuku ya Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF).

Aidha, uzalishaji wa samaki umeongezeka hadi kilogramu 600 kwa miezi tisa kutoka kilogramu 100 za awali.

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ilisema Mkurugenzi wa Kampuni ya RiverBanks Fish Farms, Pius Nyambacha alisema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya mafunzo ya kuendeleza ujuzi kuhusu ufugaji wa samaki kwa wawakilishi kutoka Benki ya Dunia ambao ni wafadhili wa SDF.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kupitia ruzuku ya mafunzo hayo, RiverBanks Fish Farms ilipata ufadhili wa Sh milioni 131.2 kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya ujuzi kuhusu ufugaji wa samaki.

Fedha hizo zilisaidia kuboresha miundombinu ya uzalishaji vifaranga vya samaki na kufugia, kuboresha na kujenga ofisi, kununua vifaa vya kisasa vya ufugaji pamoja na kuendesha mafunzo kwa vijana na wanao awake kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Rungwe.

"Lengo lilikuwa ni kutoa mafunzo na elimu kuhusu ufugaji samaki kwa watu 400 lakini kutokana na mwikio kuwa mkubwa, tulifanikiwa kufundisha watu 427 kwa kipindi cha miezi mitatu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye alisema lengo la mfuko ni kuwezesha vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kuajiriwa au kujijiri.

Wawakilishi kutoka Benki ya Dunia na viongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na TEA walifanya ziara katika kampuni hiyo kuona hatua ya utekelezaji wa mradi wa mafunzo ya kuendeleza ujuzi wa ufugaji samaki.